MAENDELEO TANGU WAD 2008

Dr Fatma MRISHO, Mwenyekiti Mtendaji, Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Tanzania (TACAIDS)

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa

Waheshimi wa Mawaziri

Waheshimiwa *Commissioners* waTume ya Kudhibiti UKIMWI

Mwenyekiti wa TACAIDS alienitangulia (Maj. Gen. Retired Herman Lupogo)

Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na UKIMWI (NACOPHA)

Viongozi wa dini Wageni Waalikwa

WanaTanga

Niungane na walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza Mkuu wa Mkoa waTanga watendaji wake kwa maadhimisho ambayo yamefana sana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa niaba yaTume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, nakushukuru sana Mhe Mgeni Rasmi kwa kuwepo kwako hapa ijapokuwa sote tunafahamu ukubwa na uzito wa majukumu yako, tumefarijika sana.

Naomba, kwa kifupi niongelee maendeleo na mabadiliko tunayoyaona kwenye UKIMWI kama suala linalohusu Sekta mbali mbali

Tanzania imeendelea kuona mafanikio mengi yaliyojitokeza hasa kwenye uelewa zaidi wa vyanzo, vichocheo na namna ya kupunguza maambukizo mapya ya UKIMWI.

La kwanza: Mwitikio, hasa kwa rika la vijana umekua mkubwa, dalili ni kuwa vijana ndio wanaofanya maambukizo kupungua kwa asilimia 2% - shukurani na pongezi nyingi kwa vijana wenyewe na asasi zisizo za serikali, sekta binafsi na viongozi wa Dini

kwa kuungana na serikali kufikisha ujumbe kwa vijana wa Tanzania kwakupitia, shule, vyuo, vyuo vikuu, mikusanyiko ya vijana, mbio za Mwenge, kutumia sinema, nyimbo, usanii, michezo na vivutio vingine vya vijana.

Mheshimiwa mgeni rasmi,

Pili: Uelewa wetu wa UKIMWI na jinsi unavyoathiri uchumi wetu umeongezeka kufikia 98% baada ya kupata matokeo ya utafiti wa UKIMWI unavyowaathiri walemavu, wavuvi, wafanyakazi machimboni na wajenga barabara na miundombinu mingine, kazi ambazo zinawafanya kwa vipindi virefu wanajamii kuwa mbali na familia zao. Ufahamu huu umeongeza hoja ya UKIMWI kuwa ni moja ya maeneo muhimu ya MKUKUTA.

Tatu: Watu wengi zaidi wamejitokeza kupima kufikia asilimia 37% kwa wanawake na asilimia 27% kwa wanaume – tunayoyaona hapa uwanjani kwenye mabanda ya upimaji ni mfano hai. Ijapokua unyanyapaa bado ni kikwazo kikubwa, kuna wengi

ambao wamejiweka wazi kuhusu hali zao. Inaleta faraja kupata taarifa, na kuona tunapotembelea Halmashauri, miji na vijiji –kwamba kuna baadhi ya maeneo ambapo Watu Wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI, wamepata mafunzo mafupi na wanaunga mkono nguvu za Serikali kutoa huduma za UKIMWI majumbani, shuleni, elimu kwa wajenzi wa barabara, kwa wauza bar na kwa wafanyikazi kwenye nyumba za wageni. Miezi miwili iliyopita tulipokuwa Rukwa tuliliona hili na likaturidhisha sana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

La nne: Sekta zinazidi kuongeza nguvu katika kukabiliana na tatizo la UKIMWI mahala pa kazi, sasa hivi jumla ya Sekta 47 zinatekeleza program za UKIMWI mahala pa kazi, pongezi kubwa – sio kwa upendeleo bali kwa kutekeleza na kutoa taarifa (*admittedly* wakati mwengine kwa mbinde)kwa sekta zifuatazo:

- Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kupanua huduma za afya kama Mhe Waziri atakavyoeleza kwa ukamilifu. Upanuzi wa Afya ya msingi utaongeza zaidi ufikiwaji wa wananchi na huduma hizi.

- Wizara ya Kilimo ambayo ilikuwa ya kwanza kutayarisha mkakati wa kukabiliana na UKIMWI kwa wafanyakazi wao na pia kwa wakulima wanaokutana na wafanyakazi wao wa ugani. Mkakati huo unalenga kama kilimo, uvuvi, ufugaji na misitu. Tume na Wizara ya Kilimo tukishirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo (FAO) tunaupitia kwa dhamira ya kuweka mkazo zaidi kutumia taarifa za tafiti na maendeleo ya karibu ni la muhimu zaidi nikuweza kutumia kaulimbiu na dhamira ya Kilimo kwanza ambayo itawezekana tu kama wakulima, wafugaji, dalali, wanunuzi na wauzaji wa mazao na mifugo watakua wana elimu na stadi za kujikinga.

- *Ofisi ya Rais, Menejmenti na Utumishi wa Umma* kwa kuona umuhimu wa kutilia mkazo UKIMWI kwa afya na uhai wa wafanyikazi wa Serikali sasa wako kwenye mchakato wa kuimarisha waratibu wa UKIMWI kwenye MDAs

- *Uhamiaji* imefanya vizuri kwa kutoa taarifa na elimu kupitia vipeperushi kwa wanao ingia nchini *kupitia* mipaka yetu yote ya nchi.

- *Magereza* wanapanua huduma za kutoa elimu ya kujikinga UKIMWI kwa wafungwa – ilianzia Mkoa wa Morogoro kwa majaribio na sasa inatanuka Lindi na Mtwara na kuendelea.

- *Madhehebu ya Dini* ya na mikakati maalum ya kuelimisha waummini wao; ikiwemo elimu ya UKIMWI – kwa wenyendoa, vijana, wanatoa huduma za Afya na matunzo majumbani pamoja ya ulezi na matunzo ya watoto yatima

- Sekta binafsi nayo inafanya kazi nzuri, sio tu kwa kutoa elimu na huduma kwa wafanyikazi wao, bali pia kusaidia rasilimali, uzoefu na elimu

ya kinga ya UKIMWI, na huduma kwa wananchi wanao wazunguka. Kuna kampuni za ujenzi wa barabara sasa, (baada ya ushawishi wetu) ambazo zinatenga asilimia (3%) ya fedha ya barabara kwa huduma za kinga na tiba ya UKIMWI. Wengine wanatoa fedha kwa utafiti na kuwapa asasi za kiraia kupanua huduma

- Huduma vijijini na mijini kupitia TASAF, ambao kwa maoni yetu wanafanya kazi nzuri sana kufikisha elimu na matunzo ya UKIMWI kwa jamii za Mikoa 17, kupitia jumla ya miradi 1,953, ambayo asilimia themanini na nne (84%) imeishapatiwa fedha shilingi karibu bilioni tisa (8.9 bilion shillings)

- Uwazi na matumizi bora ya fedha na rasilimali za UKIMWI umeongezeka. Hali hii itazidi kuboreka kwa vile mfumo wa taarifa wa TAMISEMI sasa utaanza kuingiza pia asasi zisizo za serikali na zilizo nje ya sekta ya afya. Bado tunawaomba wananchi watumie utaratibu na vyombo viliopo kutoa taarifa za matumizi mabaya ya rasilimali za UKIMWI ili zichunguzwe

na hatua zichukuliwe. Ufahamu wa dhana ya walengwa nao pia unaongezeka, kuwa walengwa ni wote walio Tanzania – wanalengwa wasipate maambukizo na waliopata maambukizo wapate huduma zitazowawezesha kuwa na maisha ya afya, na matumaini.

La Tano (na la mwisho): Tanzania inaaminika na inapewa hadhi kubwa Kimataifa kwa mwenendo wa shughuli za UKIMWI zinavyoendeshwa. Tumetembelewa naTume ya Kudhibiti UKIMWI Kenya, ni moja ya nchi 26 zilizoalikwa kuchangia uzoefu wetu wakukabiliana na masuala ya UKIMWI na jinsia. Mwenendo huu mzuri umeiwezesha nchi kupata misaada mingi kihali na mali kutoka kwa wenzetu wafadhili wakiongozwa na Serikali ya Marekani ambayo inafadhili shughuli za UKIMWI kwa kiwango cha asilimia arubaini na mbili (42%).

Mheshimiwa mgeni rasmi,

Mafanikio ni mengi, lakini bado changamoto zipo. Zinazoongoza ni gharama kubwa za huduma za Kinga kwa wale 94% ambao hawana

maambukizo,Tiba kwa waliopima na kuhitaji tiba – idadi ambayo inaendelea kukua. Changamoto nyingine ni utambuzi na matunzo ya yatima ikifuatiliwa na changamoto sugu kubwa ya unyanyapaa.

Mwisho, **Mheshimiwa mgeni rasmi**, athari ya UKIMWI kwa maendeleo ni dhahiri, lakini athari ya UKIMWI kwa wanawake, mzigo wa maambukizi, uuguzi, na wimbi la kunyang'anywa mali endapo mwenza amefariki au hata anaumwa sana ni la kusikitisha na la kufanyiwa kazi zaidi. Serikali imeweka sheria, lililobaki ni ombi kwa jamii kutoyafumbia macho unyanganyi huu, ukemewe na uwekwe wazi kwa viongozi wa vijiji, mitaa, viongozi wa dini, na njia zote za salama zitumike, familia hizo zisikose haki zao stahili.